# Rais Samia aipandisha hadhi Kibaha

Kisima Cha Maarifa

# FIKRA PEVU

fikrapevu @fikrapevu @fikrapevu

Tovuti: www.fikrapevu.co.tz | ISSN 3456-1679 Toleo Na.11 Fikra Pevu Jumanne Januari 28, 2025 Bei Tsh. 1,000 | Ksh.

# Katibu wa UN ampongeza Rais Samia

- Avutiwa na uwekezaji sekta ya Madini
- Aonesha utayari wa kusaidia VISION 2030



# Dk.Biteko azindua Mkutano wa Nishati



## TRC yaongeza safari za Treni

# Katibu wa UN ampongeza Rais Samia

NA MWANDISHI WETU,

**NAIBU Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa(UN)Amina Mohamed ameipongeza serikali ya Tanzania chini ya uongozi wa Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa mkakati wa kufanya utafiti wa kina wa kijiolojia na utafutaji madini nchini.**

Naibu Katibu Mkuu Amina Mohamed ameyasema janao wakati wa mkutano wa pembeni wa Mkutano wa Nishati alipokutana na Waziri wa Madini Anthony Mavunde.

"Naipongeza Tanzania chini ya uongozi wa Rais Samia ambao umekuja na ubunifu mkubwa katika maeneo mbalimbali.Mpango wa kufanya utafiti wa kina kupitia Vision2030 ni mpango ambao tunauunga mkono kwa kuwa una lengo la kubaini madini ambayo mnayo na hivyo kujipanga vyema juu ya uvunaji wa madini hayo.

Dunia hivi sasa ina mahitaji makubwa ya madini mkakati,Tanzania imebarikiwa kuwa na madini hayo kwa uwingi hivyo suala la uongezaji thamani,utunzaji wa mazingira na kulinda jamii zinazoishi katika maeneo ya uchimbaji wa madini ni vyema yakazingatiwa wakati wa uandaaji wa mkakati maalum wa uvunaji wa madini ya kimkakati.

Umoja wa Mataifa kupitia programu zake mbalimbali za utunzaji wa mazingira ipo tayari kuunga mkono jitihada hii kubwa ya serikali ya Tanzania"amesema Mhe. Mohamed.

Akizungumza katika mkutano huo,Waziri wa Madini,Anthony Mavunde,alisema, kipaumbele cha sekta ya Madini kwa hivi sasa ni kufanya utafiti wa kina ili kuiwezesha nchi kupata taarifa za kiwango na ubora wa madini iliyonayo.

Amongeza kwamba, utafiti wa kina utaleta matokeo chanya kwenye maeneo ya kijamii na kiuchumi na hivyo kusaidia kuchochea maendeleo ya Tanzania,kwakuwa pamoja na mafanikio yote ya kwenye sekta ya madini eneo ambalo limefanyiwa utafiti ni asilimia 16% ya eneo la nchi nzima.

# DK.Biteko azindua mkutano wa nishati

NA MWANDISHI WETU,

**NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati,Dk. Doto Biteko, amesema Afrika inapaswa kutumia fursa zote za nishati zinazopatikana ili kupunguza upungufu wa umeme unaoathiri takriban Waafrika milioni 571.**

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana,katika ufunguzi wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu nishati, Dk.Biteko alibainisha kuwa bara hilo linahitaji mkakati wa pamoja kufikisha huduma ya umeme kwa Waafrika milioni 300 ifikapo 2030.

Alisema,Tanzania imepiga hatua kubwa,kutoka kuzalisha megawati 21 za umeme mwaka 1960 hadi megawati 3,160 sasa huku asilimia 61 ya nishati hiyo ikiwa safi.

Biteko alisema,mtandao wa umeme umeunganishwa na nchi jirani kama Kenya na Rwanda ambapo alisisitiza umuhimu wa uwekezaji wa kimkakati katika sekta ya nishati ili kuchochea maendeleo ya viwanda, madini, na huduma za hoteli barani Afrika.

Mkutano huu pia unaakisi juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye ameonyesha dhamira thabiti katika kuimarisha upatikanaji wa nishati safi kwa Watanzania. Rais Samia amekuwa kinara wa kampeni za nishati safi ya kupikia, akihamasisha matumizi ya gesi asilia na teknolojia endelevu kwa lengo la kupunguza utegemezi wa kuni na mkaa, ambao umechangia uharibifu wa mazingira.

Aidha mkutano huo wa Nishati Afrika ni fursa kubwa kwa Tanzania kuonyesha nafasi yake kama mshirika wa maendeleo ya bara. Kwa dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha upatikanaji wa nishati safi, Tanzania inajipanga kuwa mfano wa kuigwa katika mapinduzi ya nishati Afrika.

Kwa kuwa mwenyeji wa mkutano huu, Tanzania inasimama si tu kama jukwaa la maamuzi ya kimkakati, bali pia kama mshirika wa kweli wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa Bara la Afrika. Njia ya kuelekea Mission 300 inafunguliwa, na Dar es Salaam inakuwa kitovu cha mageuzi haya.

# Ded Mnasi azindua kitabu malezi ya watoto

NA HUSNA NASSORO

**MWANDISHI wa kitabu cha Elimu na Malezi kwa Watoto Katika Zama za Kidijitali ambaye pi ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro Dkt. Haji Mnasi amezindua kitabu hicho katika kijiji cha Kitangari Sokoni kilichopo wilayani Newala mkoani Mtwara.**

Uzinduzi wa kitabu hicho umefanya juzi katika Uwanja wa Mpira Shule ya Msingi Kitangari B.Dkt.Mnasi amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kumuamini huku akisema licha ya kuwa na majukumu mengi ya kiserikali ila aliwiwa kuandika kitabu hicho kutokana na kasi kubwa ya ukuaji wa utandawazi ambao umeelezwa kuaathiri mila na tamaduni za taifa.

"Kitabu hicho kinaenda kuwa suluhisho katikati zama hizi za utandawazi na ukuaji wa teknolojia", alisema,Dkt. Haji Mnasi.



Hivyo Dkt. Haji Mnasi amewataka wazazi, walezi pamoja na jamii kupata nakala za kitabu hicho ili kuwasaidia watoto katika namna bora ya kujifunza na kupata elimu pamoja na malezi yaliyo bora ili kukuza taifa lenye maadili mema, uchapakazi kama ambavyo maono ya Rais Samia Suluhu yamekuwa yakijikita katika kusisitiza ujenzi wa jamii bora na kizazi salama cha kesho.



# Rais Samia aipandisha hadhi Kibaha

NA MWANDISHI WETU

**WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais -TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa, ameweka wazi kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ameridhia Halmashauri ya Mji wa Kibaha kupandishwa hadhi na kuwa Manispaa.**

Mchengerwa ameeleza kuwa taratibu za mwisho zinafanywa, na kutatangazwa rasmi kuwa Manispaa hivi karibuni.Ameeleza hayo katika mkutano wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoani Pwani uliofanyika Mailmoja, Kibaha.

Mkutano ulioandaliwa kupongeza na kuunga mkono azimio la mkutano Mkuu maalum wa CCM uliofanyika Dodoma, kumchagua Mwenyekiti CCM Taifa Dkt Samia Suluhu Hassan kugombea kiti cha Urais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Mchengerwa alisema,tangu Rais Samia aingie madarakani, tayari ameunganisha vitongoji kuwa vijiji na vijiji kuwa miji kulingana na vigezo na utaratibu ulio wazi.

"Kwa namna mji wa Kibaha ulivyokuwa, hakuna sababu mji huu usiwe Manispaa. Rais Samia kwa kushirikiana na viongozi wa mkoa, wilaya, na jimbo, ameleta maendeleo makubwa Kibaha na Mkoani Pwani, na hayo ni manufaa ya vizazi vijavyo," alisema Mchengerwa.

Alifafanua zaidi kuwa hakuna anayekataa kwa macho kwamba Rais Samia amefanya kazi inayoonekana na ameacha alama katika sekta zote, huku wananchi wakiwa mashahidi wa maendeleo hayo.

Kwa mujibu wa Mchengerwa, ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Rufiji na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa wa Pwani (MNEC), Mkoa huo ni miongoni mwa mikoa inayoongoza kwa kura, na tutaakikisha hakuna kura inayopotea wakati wa uchaguzi.

MNEC huyo aliwataka madiwani, wabunge, na wanachama wa CCM kuendelea kukisemea chama kwa kueleza utekelezaji wa ilani na miradi iliyotekelezwa.

Naye Mbunge wa Jimbo la Kibaha Mjini, Silvestry Koka, alifurahi na kuishukuru Serikali kwa uamuzi huu baada ya maombi yao ya muda mrefu ya kuhakikisha mji wa Kibaha unakuwa Manispaa.

"Katika mji wetu, yaliyofanyika ni mengi kama maajabu, lakini Rais Samia anafanya maajabu zaidi. Mfano, mwaka 2010 wakati naingia madarakani, lami pekee ilikuwa kuanzia Tamco – Hospitali ya Tumbi hadi Pichandege. Leo hii, karibu kila kata ina barabara ya lami na ambazo hazijakamilika zinakwenda kutandazwa lami katika kata zote," alibainisha Koka.

Koka alieleza kuwa kwa sasa Kibaha ina hospitali ya wilaya Lulanzi, vituo vya afya, umeme kila kona, miundombinu ya barabara, na ujio wa barabara sita katika barabara kuu ya Morogoro. Pia, nishati ya umeme, maboresho katika sekta ya elimu, na maji safi vimeendelea kutekelezwa, ambapo imebakia kata ya Pangani ambayo kuna mradi unaendelea, na ukikamilika kero hiyo itakuwa historia.

"Maendeleo haya yote ni matunda ya jitihada zilizofanywa na Serikali, madiwani, jimbo, na usimamizi wa CCM, na ndio sababu ya kupanda hadhi Halmashauri yetu kuwa Manispaa," aliongeza Koka.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Pwani, Mwinshehe Mlao, alitoa tamko la Mkoa wa Pwani kuunga mkono Mkutano Mkuu maalum wa CCM kumchagua Mwenyekiti wa CCM Taifa kugombea nafasi ya Rais kwa tiketi ya CCM katika uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Pia, walimpongeza Emmanuel Nchimbi kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza kupitia CCM katika uchaguzi huo.Kadhalika, Mlao amempongeza Rais wa Zanzibar, Hussein Mwinyi, kuwa mgombea wa nafasi ya Rais kupitia CCM Zanzib

# TRC yaongeza safari za Treni

NA MWANDISHI WETU

**SHIRIKA la Reli Tanzania (TRC) limetangaza kuongeza huduma za treni za mijini kati ya Stesheni ya Kamata na Pugu, jijini Dar es Salaam kwa siku kuanzia jana kutokana na kufungwa kwa baadhi ya barabara za kuingia katikati ya jiji kutokana na mkutano wa nishati wa wakuu wa nchi za Afrika.**

Kwa mujibu Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano, Fredy Mwanjala imezitaja treni hizo kuwa ni ya Stesheni ya Kamata na Pugu. Mwanjala amesema treni zilizoongezwa ni ya saa 12.00 asubuhi kutoka Stesheni ya Kamata na treni ya saa 12.05 jioni kutoka Stesheni ya Pugu.

"Shirika la Reli Tanzania linapenda kuwatangazia kuwa kutokana na kufungwa kwa barabara za kuingia katikati ya Jiji la Dar es Salaam kufuatia mkutano wa nishati wa wakuu wa nchi za Afrika, shirika limeongeza treni mbili za mjini kati ya Stesheni ya Kamata na Pugu, Jijini Dar es Salaam kwa siku ya Januari 27 na 28, 2025," imeeleza taarifa hiyo.

Hata hivyo, Mwanjala alisema pamoja na hatua hiyo ratiba za awali za treni zitabaki kama kawaida.

# Unajua sababu zinazomfanya mwanamke asifike kileleni?



**KUNA sababu mbalimbali zinazoweza kumfanya mwanamke asifike kileleni (orgasm) wakati wa tendo la ndoa au mahusiano ya kimapenzi. Sababu hizi zinaweza kuwa za kimwili, kisaikolojia, kihisia, au za mazingira. Hapa kuna baadhi ya sababu kuu:**

**1. Sababu za Kisaikolojia**

Msongo wa mawazo: Wasiwasi wa maisha, kazi, au matatizo ya kifamilia yanaweza kuathiri hamu ya mapenzi na uwezo wa kufikia kilele.Hofu au aibu: Hofu ya kushindwa, kutokujiamini, au aibu kuhusu mwili wake inaweza kumzuia mwanamke kufurahia tendo kikamilifu.

Matatizo ya kihisia: Mfano ni unyanyasaji wa kihisia, matatizo ya uhusiano, au hisia za kutothaminiwa.Matukio mabaya ya zamani: Mfano ni historia ya unyanyasaji wa kijinsia au uzoefu mbaya wa awali.

**2. Sababu za Kimwili**

Kutokuwa na hisia za kutosha: Kukosa utangulizi (foreplay) wa kutosha huathiri mwili wa mwanamke na kumfanya asijisikie tayari.Matatizo ya kiafya: Magonjwa kama kisukari, shinikizo la damu, au matatizo ya homoni yanaweza kuathiri uwezo wa kufikia kilele.

Matumizi ya dawa: Dawa fulani, kama za kuzuia msongo wa mawazo, dawa za usingizi, au baadhi ya vidonge vya uzazi, zinaweza kupunguza hamu ya mapenzi au uwezo wa kufikia kilele.Maumivu wakati wa tendo: Ikiwa mwanamke anahisi maumivu, anaweza kushindwa kufurahia tendo kikamilifu.

**3. Sababu za Kihisia**

Ukosefu wa mawasiliano na mpenzi: Mawasiliano hafifu kuhusu mapenzi au kile kinachomfurahisha mwanamke kinaweza kusababisha kutokufika kileleni.Mahusiano yenye matatizo: Kutoelewana, migogoro, au kutoaminiana katika mahusiano huathiri hamu ya mapenzi.

4. Sababu za Mazingira

Ukosefu wa faragha: Kukosa mazingira ya utulivu au kuhisi kuna watu karibu kunaweza kumfanya mwanamke ashindwe kuzingatia tendo.Uchovu: Uchovu wa mwili au akili huathiri hamu ya mapenzi.

**Jinsi ya Kushughulikia Tatizo**

1. Kuzungumza na mpenzi: Kuwasiliana wazi kuhusu hisia, matarajio, na kile kinachokufurahisha ni hatua muhimu.

2.Utangulizi wa kutosha: Hakikisha kuna muda wa kutosha wa kujenga hisia kabla ya tendo.

**3.Kuwasiliana na daktari:Ikiwa kuna matatizo ya kiafya au matumizi ya dawa, ni vyema kumshirikisha daktari.**

**4. Usaidizi wa kisaikolojia: Kushirikiana na mshauri wa mahusiano au mtaalamu wa saikolojia inaweza kusaidia.**

**5. Mazoezi na afya bora: Mazoezi ya mwili na kula chakula bora yanaweza kuboresha mzunguko wa damu na afya ya mwili kwa ujumla.**



# Kwanini Waasi wa M23 wanautaka mji wa Goma?

**MJI wa Goma ulio mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo umekuwa tena kitovu cha mzozo wa kikanda uliodumu kwa miongo kadhaa. Mapigano kati ya kundi lenye silaha linalojulikana kwa jina la M23 na Jeshi la Congo yamezidi katika eneo hilo, na kuwafukuza zaidi ya watu 400,000 kutoka makwao tangu mwanzoni mwa mwaka huu. Lakini kwanini Goma - mji mkuu wa mkoa huo - ni mji unaopiganiwa ?**

**M23 ni akina nani?**

Kundi la M23 ni kundi lenye silaha ambalo lilijitenga na jeshi la Kongo miaka kumi iliyopita kwa madai ya kuwalinda Watutsi ambao kwa muda mrefu walikuwa wakilalamikia mateso na ubaguzi.

Wataalamu wa Umoja wa Mataifa wanasema kuwa kundi hilo linaungwa mkono na nchi jirani ya Rwanda, ambayo pia inaongozwa na Watutsi, jambo ambalo serikali ya Rwanda imekuwa ikikanusha mara kwa mara. Rwanda imesema hapo awali kwamba mamlaka nchini DR Congo inashirikiana na baadhi ya waliohusika na mauaji ya kimbari ya mwaka 1994 dhidi ya Watutsi na Wahutu wenye msimamo wa wastani.

Mwaka 2012,waasi waliikalia Goma kwa siku 10 kabla ya kuiacha kufuatia shinikizo la kimataifa.Baada ya hayo, kundi la M23 lilipata pigo baada ya kushindwa vibaya na jeshi la Kongo likisaidiwa na Jeshi la kimataifa ambalo lilishuhudia kufurushwa kwao kutoka nchini humo.Wapiganaji wa M23 kisha walikubali kushirikishwa tena katika jeshi kwa ahadi kwamba Watutsi watalindwa.Lakini,mwaka 2021,kundi hilo lilichukua tena silaha, likisema ahadi zilikuwa hazijatimizwa.

M23 tangu wakati huo wamechukua udhibiti wa maeneo mengi zaidi katika eneo la mashariki kuliko hapo awali. Wataalamu wa Umoja wa Mataifa wanasema Rwanda ina hadi wanajeshi 4,000 wanaofanya kazi pamoja na M23 Mashariki mwa Kongo DR.

**Eneo la Goma**

Likiwa kwenye ufuo wa kaskazini mwa Ziwa Kivu kwenye mpaka wa Rwanda, Goma daima imekuwa kitovu muhimu cha kisiasa na kibiashara.Mji huo una watu zaidi ya milioni moja na kuufanya kuwa moja ya miji yenye watu wengi zaidi Kongo. Kutokana na udongo wake wa volkeno, wenye rutuba kihistoria mji huo umekuwa kituo cha biashara chenye shughuli nyingi na nchi jirani ya Rwanda.

Goma ni mojawapo ya miji mikuu ya uchimbaji madini inayosambaza madini yanayohitajika sana kimataifa kama vile dhahabu, bati, kobalti na koltani na ina barabara muhimu za kimkakati za usafiri wa barabarani na angani.Pia ina kambi kubwa ya walinda amani wa Umoja wa Mataifa suala ambalo limevutia biashara nyingi, mashirika ya kimataifa na balozi.

Utajiri wa Goma

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo inakadiriwa kumiliki asilimia 70 ya madini ya cobalt duniani, madini muhimu katika kuwezesha betri za lithiamu-ion katika simu za mkononi, magari ya umeme na aina nyingi za sigara za kielektroniki.

**Je,Goma ikitekwa**?

Rais wa Kongo Félix Tshisekedi mwaka 2023 anasema kuwa "Goma haitatekwa kamwe".Ahadi zake za kuhakikisha kuwa mji huo hauna waasi zilikuwa juu kwenye orodha yake ya ahadi kwa watu wa Kongo,ikimaanisha kutekwa kwa Goma kungemuathiri kisiasa kiongozi huyo aliyechaguliwa tena.

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo imekata uhusiano wote na nchi jirani ya Rwanda, jambo ambalo limesababisha onyo kutoka kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres kwamba mzozo wa sasa unaweza kuhatarisha kuongezeka kwa vita vya kikanda.Kuongezeka kwa mzozo kunaweza pia kusababisha uhaba wa rasilimali za kibinadamu ambazo tayari zimepungua kutokana na machafuko mengine.


Wakati M23 inasonga mbele katika eneo la Mashariki,maelfu katika vijiji vidogo wanayahama makazi yao na kuelekea katika hospitali za karibu huko Goma, jambo ambalo linawalemea.

Shirika la kutetea haki za binadamu la Human Rights Watch limeonya juu ya kuongezeka kwa hatari kwa raia huku Jeshi la Kongo likipambana na waasi wa M23.Kundi la misaada ya kibinadamu linashutumu pande zote mbili kwa kutekeleza unyanyasaji mkubwa dhidi ya raia.



# Kumekucha 'Valentine Day' mapango Amboni

NA PHILOMENA MBIRIKA, TANGA



**MAMLAKA ya Hifadhi ya eneo la Ngorongoro (NCAA)imezindua Kampeni ya kuhamasisha utalii wa ndani katika mapango ya Amboni Tanga kuelekea sikukuu ya wapendanao inayoadhimishwa kila mwaka Februari 14.**

Kampeni hiyo imezinduliwa Januari 26 mwaka huu na Mkuu wa Wilaya ya Tanga,Japhari Kubecha,ikiwa na kauli mbiu isemayo"Diko la Amboni: Furaha ya Asili,Utajiri wa Urithi,"ambapo pamoja na kuhamasisha utalii wa ndani kampeni hiyo inalenga kukuza uchumi wa wajasiriamali wadogo katika mkoa wa Tanga.

Kubecha anasema uongozi wa NCAA umefanya juhudi kubwa za kuhamasisha utalii wa ndani katika mapango hayo na kutoa rai kwa wananchi ndani na nje ya Mkoa wa Tanga kujenga utamaduni wa kutembelea vivutio vilivyopo ndani ya nchi.

"tunatambua juhudi za pekee zinazofanywa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kuhakikisha kuwa utalii mambo kale na urithi wa utamaduni unaendelea kuwa kivutio bora cha watalii nchini, kutokana na hili naomba nitoe rai kwa wananchi wote ndani na nje ya mkoa wa Tanga kuhakikisha kuwa siku ya Wapendanao tunakutana hapa Amboni". anasema Kubecha.

Kwa upande wake Kamishina Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi, NCAA anayesimamia huduma za utalii na masoko, Mariam Kobelo anasema kwamba kuelekea siku hiyo NCAA itatoa nafasi kwa wakazi wa Tanga kushiriki kwenye shughuli mbalimbali zitakazofanyika hapo ili kuendelea kutoa hamasa na kuongeza uwelewa wa shughuli mbalimbali za Uhifadhi zinazofanywa na Mamlaka hiyo.

"Shughuli hii ambayo tunaenda kuifanya msimu huu wa sikukuu za wapendanao itahusisha mashindano ya Upishi wa vyakula vya asili, ambayo yatafanyikia hapa amboni pamoja na kutembea ndani ya mapango na kupatiwa elimu juu ya kivutio hiki cha kipekee kilichopo katika nchi yetu" anaeleza Mariam

Aidha, Kobelo anasema,siku hiyo itakuwa nzuri na itawawezesha watanzania kushiriki, ambapo Mamlaka imeshirikiana na Kampuni ya Utalii ya Smiles Safaris ambayo itatoa huduma za kuwaleta watalii amboni kutoka mikoa ya Dar es salaam, Arusha, Kilimanjaro na Tanga ambapo gharama za ushiriki kwa kila Mkoa zitatolewa na gharama hizo zitahusisha Chakula, Malazi siku moja, viingilio pamoja na picha.

Mapango ya Amboni Tanga yanayosimamiwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) tangu mwaka 2019 yapo umbali wa Km 9 tu kutoka katikati ya Jiji la Tanga.

Mapango hayo yamefanyiwa maboresho mbalimbali ikiwemo ufungaji wa taa maalum kuwezesha mgeni kuona vivutio vilivyopo ndani ya Mapango sambamba na kuboresha njia za mapito katika eneo la ndani ya mapango hayo ambapo kwa sasa eneo hilo linapokea wageni zaidi ya 30,000 kwa mwaka.



# Dk. Samia na rekodi ya kipekee Mkutano wa Nishati Nchi za Afrika

NA HUSNA NASORRO

**MKUTANO wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika umeanza jana jijini Dar es Salaam kwenye Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam huku mwenyeji wake Rais Dk.Samia Suluhu akiweka rekodi ya kipekee.**

Takwimu zinaonesha jumla ya Wakuu wa nchi 25 za Afrika wanahudhuria Mkutano huo hatua ambayo inamfanya Dk.Samia kuwa Rais wa kwanza aliyepokea idadi kubwa ya viongozi wa ngazi ya juu tangu ipate uhuru.

Mara ya mwisho Tanzania kupokea ugeni mkubwa wa wakuu wa nchi za Afrika ilikua mwaka 1999 wakati wa Kifo cha Baba wa Taifa,Hayati Julius Kambarage Nyerere lakini hivi karibuni ilikuwa mwaka 2019 wakati Wakuu wa Nchi 15 walipohudhuria Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Nchi ambazo Wakuu wa Nchi zao wanashiriki Mkutano huo kutoka Algeria,Comoro, Liberia, Lesotho, Botswana, Kenya, Ghana, Gabon, Sierra Leone, Ethiopia, Sudan na Malawi.Nyingine ni Zambia, Somalia, Guine Bisau, Burundi, Mauritania, Kongo Brazzaville, Madagascar, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Libya, Nigeria, Djibouti na Gabon.

Makamu wa Rais watakaoshiriki ni kutoka Gambia na Benin,Mawaziri Wakuu kutoka Cote d'Ivoire, Uganda, São Tomé and Príncipe na Equatorial Guinea na Naibu Mawaziri Wakuu ni kutoka Eswatine na Namibia.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati na Madini,Doto Biteko,anasema,Tanzania imepata wenyeji wa Mkutano huo kutokana na juhudi za Rais Dk.Samia Suluhu Hassan kuifungua nchi katika masuala ya Diplomasia lakini kivutio kingine ni kuwa kisiwa cha amani.

Anasema,pia waaandaji wa Mkutano huo Benki ya Dunia(WB) wameichagua Tanzania kutokana na kuwa nchi ya Afrika iliyo mstari wa mbele katika mpango wa kupeleka umeme vijijini.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mahmoud mkutano huo ni mwendelezo wa matunda ya diplomasia ya Tanzania ambapo Serikali imejipanga kuhakikisha kuwa Tanzania inaendelea kutangazika barani Afrika na duniani kwa ujumla.

Tanzania inatarajia kuwa Mwenyeji wa Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Nishati baada ya Dk.Samia kuridhia ombi la Benki ya Dunia (WB) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu Mhandisi Innocent Luoga,Mkutano huo utahusisha Wakuu wa Nchi 54 katika Bara la Afrika, MaRais wa WB, AfDB, Umoja wa Afrika, Mawaziri wa Fedha na Mawaziri wa Nishati.

Akielezea chimbuko la Mkutano huo, Mhandisi Luoga anasema takwimu zinaonesha kuwa, takribani Waafrika milioni 685 hawajafikiwa na huduma ya umeme hadi sasa kati ya Waafrika zaidi ya Bilioni 1.


Benki ya Dunia kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo Afrika wamekuja na Mpango Mahsusi ujulikanao kama Mission 300 ambao umelenga kuharakisha upatikanaji wa umeme kwa Waafrika Milioni 300 ifikapo 2030.

Anaeleza kuwa, Mpango huo unahusisha nchi zote za Afrika ambapo nchi 14 zimechaguliwa kuanza utekelezaji wa Mpango wa Mission 300 na nchi nyingine zitafuata.Amezitaja nchi hizo kuwa ni Tanzania, Mali, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Ivory Coast, Bukina Faso, Chad, Liberia, Madagascar, Malawi, Mauritania, Msumbiki, Niger, Nigeria na Zambia.

Tanzania imeingizwa katika Mpango huo kwa kuwa ni nchi mwenyeji wa Mkutano kwani imeshapiga hatua kubwa katika usambazaji wa umeme kwa wananchi.

Anaeleza kuwa kupitia Mpango Mahsusi wa Kitaifa wa M300 unaofadhiliwa na WB, AfDB na Wadau wengine wa Maendeleo, Tanzania itaweza kuunganishia umeme watanzania milioni 13.5 yaani karibu mara mbili ya uwezo wake katika kipindi hicho cha miaka mitano na hivyo kufanya ongezeko la wateja milioni 8.3.

Mwanadiplomasia namba Moja wa Tanzania na Rais Samia ameendelea kuonesha Nguvu yake ya ushawishi Duniani kwa kuwaleta viongozi wa Dunia kuja kushiriki. Ikumbukwe huu ni mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika ila viongozi wa Dunia pia watakuja Kwa ushawishi wa Rais Samia chini ya ajenda yake kuu ya Nishati safi Kwa Wanawake.



# WARAKA WANGU KWA KATIBU MKUU WA CCM DK. EMMANUEL NCHIMBI

NA VICTOR MAKINDA

**KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi(CCM)Ndugu Emanuel Nchimbi,pokea salamu zangu za pongezi kwa kuteuliwa kwako kuwa mgombea mwenza katika kinyang'anyiro cha Urais kitakachofanyika Oktoba mwaka huu.Kwangu CCM imepiga bao la kisigo kwa uteuzi wako.**

Ni mtu sahihi katika wakati sahihi unayekwenda kumsaidia Dk.Samia Suluhu kushinda kwa kishindo kiti cha Urais na wewe kuwa Makamu wake utakayemsaidia katika majukumu ya utekelezaji ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Hii ni mara ya pili na najitokeza hadharani kukupongeza.Mara ya kwanza ilikua

ni pale ulipoteuliwa kushika nafasi ya Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi chini ya Mwenyekiti wako Imara Dk.Samia Suluhu Hassan.

Nikiwa Mtanzania Mzalendo, mwenye mapenzi makubwa kwa nchi yangu na chama kinachotawala,nimewiwa kuandikia waraka huu muhimu kwako na wenzako chamani ambao kwa pamoja sasa mna dhima kubwa ya kuendelea kuiimarisha,kuikuza na kuiendeleza CCM ili iendelee kushika dola. Naam, dhima kubwa ya chama cha siasa ni kushika dola.

Kabla ya kwenda mbali ningependa kwanza tuirejea kauli ya Mwenyekiti wa zamani wa TANU-CCM rais wa kwanza wa Tanganyika huru baadae Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliyosema



“ Bila CCM imara nchi yetu itayumba.”

Dkt Nchimbi ninatambua kuwa ni hivi karibuni umepata uteuzi wa kuwa mgombea mwenza wa CCM huku ukiwa bado unaendelea kuitumikia nafasi yako ya Katibu Mkuu wa CCM mpaka utakapotuvusha kwenye uchaguzi Mkuu. Halikufanyika hili bila ya kuwa imani kubwa aliyonayo kwako Dk.Samia Suluhu Hassan.

Wadhifa huo muhimu wa uKatibu Mkuu wa chama kimsingi wewe ndiye Mtendaji Mkuu wa chama hiki kikongwe barani Afrika ambaye kwa sasa uimara wake unategemea sana uwezo wa utendaji wako. Kuna kitu kikubwa umekifanya katika nafasi hiyo.

Tumeiona CCM chini ya Mtendaji wake Dk.Nchimbi na sasa tunaisubiri serikali chini ya Makamu wa Rais mwenye malezi bora ya chama.

Sina chembe ya shaka juu ya uwezo wako kiutendaji, kiwango chako cha uzalendo na kiu yako ya kuhakikisha Tanzania inasonga mbele kimaendeleo.Kwa muda mfupi wa utendaji wako tumeona namna CCM ilivyoongeza idadi kubwa ya wanachama lakini chama hicho kikishinda kwa kishindo uchaguzi wa serikali za mitaa.

Wengi wameeleza jinsi wanavyokufahamu na kukumwagia sifa nyingi. Sina shaka na sifa hizo, ninaamini ni sifa zako na ni za kweli. Watanzania wanaijua vyema rekodi yako ya misimamo thabiti, kupinga vitendo vya rushwa na ufisadi, na nisema tu waumini wa vitendo hivyo viovu waliposikia kuwa umekamata usukani kwa nafasi hiyo ya Katibu Mkuu na sasa mgombea mwenza nadhani wamepatwa na kiwewe.

Ukweli ni kwamba CCM pamoja na ukongwe wake,chama hiki kingali kinakubalika kwa watanzania walio wengi na kimekuwa chama mfano wa kuigwa na vyama vingine vya siasa katika nchi mbali mbali ndani na nje ya la Afrika.

Ndiyo! CCM ina mengi mazuri ya kuigwa moja ni hili la kutunza amani na kuhakikisha inatamalaki hapa nchini.Chini ya uongozi wa CCM iliyofanikiwa kujenga mfumo imara na madhubuti kuanzia kwenye mashina, vyama vingine katika mataifa vinapata mahali pa kujifunza na kuiga namna ya uendeshaji wa nchi na serikali.

Suala la viongozi wa nchi kupokezana madaraka kwa njia ya amani pindi mihula yao inapokwisha ni miongoni mwa mambo ambayo ni nadra sana mahali pengine barani Afrika lakini Tanzania chini ya uongozi wa CCM linafanikiwa pasipo shaka yoyote.

Mwaka jana nilitembelea pwani ya Kenya, moja ya maswali ambayo nilikuwa ninakutana nayo kutoka kwa Wakenya ni kwa nini Watanzania bado wanaichagua CCM?.

Swali hilo nilikuwa ninalijibu kwa kujiamini kabisa kuwa sababu pekee ambayo Watanzania wanaendelea kuichagua CCM ni kwa kuwa chama hicho pamoja na mambo mengine mazuri ambayo kimeitendea Tanzania.Lakini uwezo wa CCM kuitunza misingi ya Utu, Umoja, mshikamano, amani na udugu ndio kiini hasa cha Watanzania kukichagua chama hicho.

Ijapokuwa nilikuwa nikiulizwa maswali kuhusu hali za maisha ya watu na umaskini unaokabili maeneo hasa ya vijijini, nilikuwa ninajibu swali hilo kwa kujiamini kabisa, nikisema kuwa ni heri ugali maharage unaokula ukiwa huru na amani kuliko wali nyama unaokula katika eneo ambalo huna hakika wa usalama wako hata sekunde moja ijayo.

Ndiyo, Tanzania ina amani, amani ya nchi hii ni miongoni mwa Tunu ambazo Mungu aliwajaaliwa viongozi waasisi wa nchi yetu. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Mzee Abeid Aman Karume walifanya jitihada za kila namna kuirithisha tunu hiyo kwa vizazi vijavyo, hiyo ndiyo sababu tungali na tunu hizo hata sasa. Wajibu wetu mkuu ni kuzilinda tunu hizo ili nasi tuzirithishe kwa vizazi vijavyo.

Nani wenye wajibu wa kulinda tunu za amani, Umoja, udugu na mshikamano wa Kitaifa? Jibu ni kwamba kila mmoja wetu anawajibu wa kuzilinda tunu hizo lakini kipekee kabisa CCM ndiyo yenye wajibu mkubwa wa kuzilinda tunu hizo kwa kuwa chama hicho ndicho kilichoaminiwa na wananchi wa Tanzania kuiongoza serikali ya Tanzania hivyo ina kila sababu ya kusimamia misingi ambayo haitateteresha tunu hizo.

Nukuu ya kauli ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, “Bila CCM imara nchi yetu itayumba inaonesha wazi jinsi Mwalimu Nyerere aliona mbali.

Alitambua kwa dhahiri kuwa jinsi alivyopandikiza sera za TANU chama ambacho msingi wake mkuu ilikuwa ujamaa na kujitegemea na jinsi ambayo yeye Nyerere na Mzee mwenzie Karume walivyoipandikiza CCM mioyoni mwa watanzania na kuwafanya watanzania waimani CCM na kukifanya chama hicho kiwe chama mfumo, ni wazi kuwa bila uimara wa CCM, Tanzania haiwezi kuwa imara.

Waasisi wa Taifa hili walifanya kila namna kuhakikisha kuwa CCM inafanya kazi muhimu ya kutunza amani, kuimarisha uchumi na kusimika misingi ya umoja na udugu miongoni mwa Watanzania.

# ‘No reform no Election’ haina afya kwa ustawi amani

NA VICTOR MAKINDA,Morogoro

**CHAMA Cha Mapinduzi(CCM) Wilaya ya Morogoro Mjini,Mkoani Morogoro, kimekitaka Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kuachana na kampeni yake ya ‘No Reform No Election’na badala yake wajielekeze kwenye siasa za maridhiano.**

Kauli mbiu hiyo ya CHADEMA chini ya Mwenyekiti wake Tundu Lissu ni kama imekaa katika sura ya kufanya maandamano yanayoweza kusababisha vurugu na uvunjifu wa amani badala ya kutumia majukwaa huru ya siasa kuwasilisha hoja zao.

Katibu wa CCM wilaya ya Morogoro Mjini,Twalib Bellege,anasema,maandamano hayajawahi kuleta suluhu bali ni chanzo cha vurugu na uvunjifu wa amani hivyo chama hicho kinatakiwa kuhakikisha kuwa hakiwi chanzo cha uvunjifu wa amani bali kinatumia uhuru uliopo wa kufanya mikutano ya hadhara ya siasa kuwasilisha hoja zao.

“ Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, ambaye pia ni Mwenyekiti wa CCM Taifa, ametoa wigo mpana kwa wanasiasa wa vyama vyote nchini, kufanya mikutano ya hadhara na shughuli nyingine za kisiasa kwa uhuru mkubwa. Ni vema vyama vya siasa vikatumia uhuru huru na sio kuandamana au kutoa kauli za vitisho vya kuzuia uchaguzi” anasema.

Anasema,chama kinachochagua maandamano kama njia ya kufikisha ujumbe ni chama mufilisi nacho huwa kimefilisika kwa hoja hivyo kinalenga kujipatia umaarufu kwa njia ya mkato ilhali madhara yake ni makubwa.

“ Niwashauri rafiki zangu, watani zangu wa Chadema kuachana na maandamano, kwani kufanya hivyo hakuwezi kuwaacha salama kwa kuwa vyombo vyetu vya dola vipo imara na timamu na kamwe haviwezi kukubali wachache wachafue umoja na amani yetu”. anasema Belege

Anasema hatua ya chama hicho kutishia kuzuia uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba mwaka huu sambamba na kufanya maandamano kama njia pekee ya kuwasilisha hoja zao inaonesha wazi kuwa chama hicho kimefirisika hoja zinazoweza kuwashawishi wananchi.

“ CCM chini ya Uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, imefanikiwa kutekeleza ilani yake ya uchaguzi kwa asilimia kubwa, ambapo sasa maisha ya Watanzania yameboreshwa vyama vya upinzani hususani Chadema wamefirisiwa hoja ndio sababu wanataka kuzuia uchaguzi na kuamini katika maandamano”.anasema.

Akizungumzia uteuzi wa Mgombea Urais wa CCM,Dk. Samia Suluhu Hassan na Katibu Mkuu wake kuwa mgombea mwenza,Belege,anasema anaupongeza Mkutano Mkuu Maalum wa chama hicho kwa kuwateua wagombea wawili hao kwani ni watu watakaoipa CCM ushindi wa kishindo.

Anasema,CCM imefanya chaguo sahihi kwa wakati sahihi kwa kumteua Dk. Nchimbi mtu ambaye utendaji wake uliotukuka katika nafasi ya Mtendaji Mkuu wa chama umewafanya wajumbe wakiongozwa na Dk.Samia wawe na imani naye.

“Uteuzi wa Dk.Samia na Dk.Nchimbi kupeperusha bendera ya CCM katika uchaguzi Mkuu umepokelewa vizuri na Watanzania wote, sisi wana CCM wa wilaya ya Morogoro mjini tunaungana na watanzania wenzetu kumpongeza kwanza Mwenyekiti na mgombea mwenza wake anasema Belege.

“ Sifa ya usikivu, ukomavu wa kisiasa, uanadiplomasia na uwepesi wake wa kuelewa na kujibu hoja kwa kutumia nguvu ya hoja na sio hoja ya nguvu ni sifa ambazo Dkt Nchimbi amejaaliwa nazo ambazo zinatutia matumaini makubwa wana CCM wa Morogoro na Tanzania kwa ujumla kuwa chama chetu kitazidi kuwa imara akiwa pembeni ya Dk.Samia kama Makamu wa Rais”anasema Belege.





# ‘No Reform na Election’ haitekelezeki

NA MWANDISHI WETU

**UKIANGALIA ratiba kwa sasa imeshakua ngumu. Hoja ya CHADEMA kutaka mabadiliko ya Katiba kabla ya kufanyika kwa uchaguzi Mkuu wa Rais,Wabunge na Madiwani Oktoba mwaka huu ni kama haitekelezi. Ni ngumu kabisa,uliosalia kabla ya kufanyika kwa uchaguzi Mkuu ni kama kufumba macho na kufumbua.**



Ni mchakato mkubwa unaohusisha mpaka Bunge. Bunge limebakiza takribani miezi sita tu kuvunjwa, hizo sheria na katiba nai atarekebisha.?Muda umebaki kidogo sana ni kama tumeshachelewa haiwezekani kabisa.Hili vuguvugu lilipaswa lianze tangu mwaka jana au mwaka juzi, kwa sasa ngoma ni ngumu.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa CHADEMA,Tundu Lissu,Kamati Kuu ya chama hicho

iliazimia kwamba ‘No reform no election’ kuelekea uchaguzi Mkuu na kwa sasa wanapigania mabadiliko ya sheria na si vinginevyo.

Ni suala la CHADEMA kuingia kwenye maridhiano na vyama vingine ili kuruhusu uchaguzi ufanyike kwa amani na utulivu. Hoja zao zinaweza kuwa zina mashiko lakini siyo kwa kuzuia uchaguzi.Ni jambo la kujipanga mwakani ndio vuguvugu lianze. Kwa dhamira njema aliyonayo Dk.Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni jambo linalowezana kufanyika.

CHADEMA waache visingizio vya kukataa kushiriki uchaguzi. Slogan yao ya No reform no election haitekelezeki kwa muda huu uliobaki kuelekea uchaguzi mkuu wa Octoba. Waache utoto na waanze kujiandaa na uchaguzi.

Tuna zaidi ya vyama 19 kama CHADEMA hawako tayari kwa uchaguzi basi hilo si suala la vyama vyote na wasilete vurugu za kijinga.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Amos Makalla anasema chama hicho kinaendelea kujipanga kwa uchaguzi ujao ambapo anabeza kauli ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) inayosema hawatoingia kwenye uchaguzi pasipo kuwa na mabadiliko ya mifumo ya uchaguzi.

Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Stephen Wasira,anasema kauli mbiu ya “No Reform, No Election” haina maana kwa sasa, akisisitiza kuwa muda wa kufanya mabadiliko ya kisheria umekwisha kutokana na uchaguzi mkuu kukaribia.

Wasira anasema badala ya kushikilia kauli hiyo,CHADEMA) wanapaswa kushiriki uchaguzi na kuhakikisha wanakubaliana na maridhiano yaliyopo.

“Kauli ya ‘No Reform, No Election’ haina nafasi kwa sasa,Rais Samia Suluhu Hassan na CCM wameonesha utayari wa mazungumzo, na bunge linakaribia kuvunjwa, hivyo hakuna muda wa kufanya mabadiliko ya kisheria yanayohitaji muda mrefu,” anasema Wasira.

Anaongeza kuwa uchaguzi mkuu wa mwaka huu, unaotarajiwa kuchagua Rais, Wabunge, na Madiwani, unapaswa kutoa nafasi kwa vyama vyote kushindana kwa hoja badala ya kutafuta visingizio.Wasira anawataka viongozi wa CHADEMA kutumia nafasi za mazungumzo zilizopo badala ya kusimamia misimamo isiyotekelezeka kwa wakati huu.

“Ni muhimu kushiriki uchaguzi na kuwa sehemu ya demokrasia badala ya kupoteza muda na kauli ambazo hazina tija kwa wananchi,” anasisitiza Wasira.

# Viwango vya Rais Samia ni ishara ya ushindi wa kimbunga

NA YUSUFU SABURA

**CHAMA cha Mapinduzi(CCM)ni miongoni mwa vyama vya siasa vilivyopata bahati kubwa sana ya kuwa na tunu ya watu wenye uwezo na weledi mkubwa sana linapokuja suala la uongozi na utawala.Hii sio mara ya kwanza kwa jambo hili kuzungumzwa lakini, nitajaribu kuzungumza kwa kadri nionavyo mimi pamoja na uzoefu wangu katika kupekuapekua haya mambo ya kimedani.**



Awamu ya kwanza iliyoongozwa na muasisi wa taifa letu Hayati Mwalimu, Julius Nyerere ndio msingi wa mambo yote mazuri tunayoyaona leo, jitihada zake katika ujenzi wa taifa zimekuwa ni wimbo kwa wanasiasa wa leo karibia wote.

Umoja na mshikamano bila kujali dini, rangi, kabila wala kipato cha mtu vimekuwa chachu ya amani katika taifa letu kwa takribani miaka sitini na tatu sasa.Haina ubishi kwamba bila amani hakuna jambo lolote la kimaendeleo linaweza kufanyika, ndio kusema kwamba, amani tunayoifaidi leo ni, zao la mawazo ya mwanaccm huyo kwani, kuunganisha makabila 120 yawe kitu kimoja sio jambo la kuchukulia rahisi hata kidogo, wenzetu wanamakabila machache lakini wameshindwa.

Kwa kutambua mchango wa awamu zote tano zilizopita, moja kwa moja tuangazie hadi awamu ya sita chini ya Rais Samia,.

Rais Samia Hassan ni kiongozi wa aina yake tunaepaswa kujivunia kama taifa. Upole wa sura yake uliwadanganya maadui zake wa kisiasa wakidhani kwamba angekuwa mpole vilevile hata katika uwanja wa mapambano ya kisiasa, matokeo yake kumbe walitaka kucheza na chui jike kama alivyowahi kujiita hapo nyuma. Viwango anavyovitumia kuliongoza taifa ni viwango vya aina yake.

Nitajaribu kuelezea ni kwa namna gani Rais Samia amekuwa ni rais mwenye viwango vya aina yake katika upande wa siasa.

Kwanza ni uthubutu wake katika kuimarisha demokrasia ya Tanzania.

Hili alianza kulionesha mara tu alipoapishwa kuwa rais wa taifa letu, hakika kwa joto la siasa lililokuwepo wakati ule na uamuzi aliochukua, kila mtu alingoja kwa hamu kuona nini kinaendelea.

Ndio kusema kwamba, kufuatia maoni ya wadau wa demokrasia waliokutana jijini Dodoma kati ya tarehe 15-17 desemba 2021, kiliundwa kikosi kazi kilichoongozwa na profesa Mukandala kutoka Chuo Kikuu Cha Dar Es Salaam, lengo likiwa ni kwenda kuangazia pembe muhimu za kugusa ili kuboresha mazingira ya kisiasa nchini.

Moja ya mapendekezo yaliyotolewa na kikosi kazi hicho tarehe 21 oktoba 2022 , ni pamoja na kuruhusu mikutano ya hadhara na mikutano ya ndani ya vyama vya siasa, kikosi kazi kilisisitiza kuwa shughuli hizo za kisiasa zifanyike bila vikwazo vyovyote. Ni tofauti na hali ilivyokuwa miaka michache nyuma kabla ya Rais Samia kuingia madarakani.

Baada ya hapo sote tumekuwa mashahidi kwamba wapinzani sasa wanafanya shughuli zao bila bughudha za kiutawala,tumeshuhudia maandamano ya amani na operesheni mbalilmbali za vyama vya siasa.Na wengine hata kujisahau kutumia majukwaa hayo kumdhihaki yeye kama Samia na sio yeye kama Rais, hii yote ni furaha iliyoletwa na rais Samia kwa wanasiasa wa upinzani.



# Utawala wa Trump, uchukuliwe kama fursa ya kujikomboa



**UTU wetu na thamani yetu, ilishuka miaka mingi, baada ya kuukumbatia ulemavu wa kusaidiwa. Tukubaliane waafrica, kuna ujinga fulani tumeushikilia, tungekuwa watu wa kuendelea kupitia misaada, tungeshatoka hapa tulipo.**

Ukweli ni kwamba, misaada mingi ya magharibi haijawasaidia walengwa wa misaada hiyo zaidi ya kuishia mifukoni mwa watu wachache.Nitamshangaa Prof. Anna Tibaijuka, kuulizia Ukimwi ulianzia wapi?.Ukimwi ulianzia Marekani,Kama ulianzia huko, ni kwa nini Umeua na kuteketeza waafrica wengi zaidi??.

Motive ya kutengeneza,hivi virusi ilikuwa ni nini?.

Ukiisoma, na kuielewa Sayansi ya Kirusi kinavyoingia,kuathiri Chembe hai ya kinga ambayo ni (Commander in chief), inayotoa amri, kwa chembei kinga nyingine, Lazima ukubaliane nami kuwa, maarifa ya binadamu ya " Genetic engineering yalifanya kazi.Dunia ina mengi ya kushangaza, Ngoja tujadiri tutawasaidiaje ndugu zetu wanaohitaji dawa hizi.

1) Kwa waafrica wote hii ni agenda yetu sote.a) Tu mobilise Resources,zetu tuwe na ushirika na wenye kupenda ushirika nasi, tujenge viwanda vyetu vya madawa, hata ikibidi kuwapeleka wana wa kiume na wa kike wa kitanzania, Kenya na nchi nyingine kupata maarifa ya juu zaidi ya kinga mwili( immunology).

b) Kila nchi inaweza kubeba jukumu moja moja, wakati Kenya wana tengeneza chanjo, sisi tujenge viwanda vya ARV.

2) Tuweke nguvu kwenye kukinga zaidi.a) Panaweza kuwa na vipimo vya kucheck kabla watu hawajaingiliana.b) Tutengeneze viwanda vya kuzalisha Condom nyingi.

C) Mtu anposhtuka kayatimba, basi guest zote ziwe na dawa za kuzuia kirusi hicho kusambaa( Post exposure prophylaxis).

d) Ngono duniani kote baadhi ya maeneo imekuwa ni commodity, basi kuwe na Priority kwenye nchi za kusaidia makundi yaliyoathirika kiuchumi, wapewe mikopo nafuu( serving disadvantaged societies),Ili ku shift equilibrium ya biashara ya ngono, kuja kwenye biashara nyingine.

3) 1,2, hapo juu zinaweza ku apply kama long term plan, short term plan ni kama hizi.a) Tupunguze matumizi.

Badala ya magari ya mil 600, tununue magari ya mil 60!, b) Tuwe na mfuko wa Taifa wa Ukimwi i) 10% ya mauzo ya kodi yaende kwenye mfuko huu.

ii)Tuhamasishe matumize ya Teleconference, badala ya kulazimisha watu kusafiri kwa kuchoma mafuta ya petrol kwa ma V8 ili tuwe na hela ya emergency kwa ajili ya mfuko huu, badala ya kuitumia kununulia mafuta ya magari.

iii) 7% ya mapato ya mashindano yote kwenye mpira iende kwenye mfuko wa Taifa wa Ukimwi.Ninajaribu kuonyesha tu kuwa, hili tatizo liko ndani ya uwezo wetu!, Trump kutunyima misaada, ni NIA njema, ya kutaka tushtuke, tutumie raslimali zetu kwa faida ya watu wetu na si vikundi vya watu.

**TUKATAE ULEMAVU WA KUSAIDIWA.**
**Isaya.**

# Kabla ya Kepteni Ibrahim Traoré, alikuwepo Kepteni Thomas Sankara

NA MWANDISHI WETU



**THOMAS Sankara, mwanamapinduzi na rais wa Burkina Faso kati ya mwaka 1983 na 1987, alikuwa zaidi ya kiongozi wa kawaida.Alikuwa sauti ya matumaini kwa Waafrika waliokuwa wakihangaika na mizigo ya ukoloni mamboleo na ubeberu wa mataifa ya Magharibi.**

Sankara, ambaye mara nyingi huitwa "Che Guevara wa Afrika," aliongoza nchi yake kwa miaka minne tu, lakini athari zake zimeendelea kuishi kwa vizazi hadi leo. Katika kipindi kifupi cha uongozi wake, Sankara aliwapa watu wa Burkina Faso maono ya nchi huru, inayojitegemea, na yenye ustawi.

Sankara aliamini kuwa elimu ni ufunguo wa maendeleo. Katika kipindi chake, aliweka juhudi kubwa kuhakikisha kuwa watoto wa Burkina Faso wanapata elimu bora. Alifanikiwa kuongeza kiwango cha wanafunzi mashuleni kwa asilimia 6, juhudi ambazo zilikuwa ngumu kwa nchi masikini yenye rasilimali chache.

Hili ni moja ya mafanikio makubwa ya uongozi wake.Sankara alizindua kampeni kubwa ya chanjo, na kufanikisha kuwapatia watoto milioni 2.6 chanjo za kupambana na magonjwa kama pepopunda, surua, na homa ya ini. Kampeni hiyo iliwasaidia maelfu ya watoto kuepuka vifo vya mapema.

Kutokana na hali ya kijiografia ya Burkina Faso, ambayo iko katika ukanda wa Sahel na mara nyingi hukumbwa na ukame, Sankara alizindua kampeni ya upandaji miti. Alifanikiwa kupanda miti milioni 10, juhudi zilizolenga kupambana na jangwa na kuhifadhi mazingira.

Sankara aliongoza harakati za kuikomboa Burkina Faso kutoka kwenye utegemezi wa Kifaransa. Alikataa misaada ya kifedha kutoka kwa nchi za Magharibi, akisisitiza kuwa misaada hiyo ilikuwa njia ya kudumisha utegemezi.

Alihamasisha wananchi kufanya kazi kwa bidii na kujitegemea.Katika jamii iliyokuwa imegubikwa na mila za kuwalazimisha mabinti kuolewa wakiwa wadogo, Sankara alianzisha kampeni kali ya kupinga ndoa za kulazimishwa.

Alitetea haki za wanawake, akiwataka kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya nchi.Sankara alijenga reli, barabara, na shule nyingi nchini humo yote haya yalifanyika bila msaada wa nchi za nje.

Miradi yake ya maendeleo iliwafanya watu wa Burkina Faso kushikamana na kuamini kuwa nchi yao inaweza kufanikisha maendeleo bila msaada wa Magharibi.

Sankara alitofautiana sana na viongozi wengine wa Afrika ambao mara nyingi walijipendelea na kujilimbikizia mali. Aliweka mfano wa uongozi wa unyenyekevu.

Alikataa picha yake kuwekwa kwenye ofisi za serikali. Alipunguza mishahara ya viongozi wa serikali, ikiwemo wake mwenyewe. Aliendesha gari ya kawaida badala ya magari ya kifahari.Alikataa kabisa matumizi ya ndege za kifahari kwa safari za nje.

Kwa mafanikio yake yote, Sankara alikabiliana na changamoto kubwa uhasama kutoka kwa mataifa ya Magharibi na wasaliti wa ndani.Mnamo Oktoba 15, 1987, Thomas Sankara aliuawa katika mapinduzi ya kijeshi yaliyopangwa na rafiki yake wa karibu, Blaise Compaoré.

Compaoré, aliyesaidiwa na Wafaransa, alichukua madaraka na kuiongoza Burkina Faso kwa miaka 27.Uongozi wake ulijaa madai ya ufisadi na ukandamizaji, tofauti kabisa na maono ya Sankara ya nchi huru, yenye haki, na yenye ustawi.

Miaka mingi baada ya kifo chake, Thomas Sankara bado anakumbukwa kama shujaa wa Afrika.Alikuwa kiongozi mwenye maono makubwa, aliyepigania heshima ya bara lake dhidi ya ubeberu wa Magharibi.Kupitia juhudi zake, alionyesha kuwa maendeleo yanawezekana hata kwa mataifa masikini ikiwa tu kuna uongozi wa kujituma, uwazi, na uzalendo.






# Ni nyakati za kila shabiki Simba kutembea kifua mbele

**ENYI mashabiki wa Simba mizimu imeniomba nije niwafikishie ujumbe wao kwenu na viongozi wa klabu yetu.Mizimu kutoka kwenye msitu wa kale wanalalamika na huu unafki ambao unaendelea na mashabiki wa klabu ya Simba wakiongozwa na kocha wao.**

Mizimu inasema ifike mahala Simba waamue kuwa wakweli wasitangaze amani huku wamebeba mapanga hii imewachukiza na kuwakera sana mizimu kutoka huko uzimuni.

Madai ya mizimu ni kuwa hii Simba sio timu tu inayojengwa ni timu ya ushindani ambayo inaweza kufanya chochote kwenye kila michuano inayoshiriki, mizimu imeenda mbali zaidi na kuuliza ni timu gani inajengwa lakini inaongoza ligi na kuongoza kundi mbele ya timu ambazo hazijengwi?

Nilipotaka kuhoji juu ya hayo malalamiko ya mizimu nilikoswa kofi na mzimu wa makamo aliyeonyesha kuwa na ghadhabu kuliko wote walioleta hayo malalamiko nikiwa usingizini.

Mizimu inasema Simba waseme tu ukweli kuwa timu wanayo na wanatamba nayo, wanauwezo wa kuchukua ubingwa wa ligi na wanauwezo wa kufika hatua ya nusu fainali kwenye michuano ya Kombe Shirikisho Barani Afrika.

Mzimu mkongwe kuliko wote uliniambia nenda kawaambie Simba kuwa hii kauli ya wanajenga timu inatosha sasa ifike hatua nao watambulike kama timu tishio kwenye michuano yote ambayo wanashiriki, na huyu Fadlu Davids awekwe ndani kwa kosa la kuwadanganya watanzania karibia million 60 kuwa haitaji lolote msimu huu zaidi ya kujenga timu tu.

Vip? Tukubaliane na mizimu kuwa Simba sasa wanataka ubingwa au Tukubaliane na Fadlu Davids kuwa anajenga timu? Imeandikwa na Hans Raphael.

fikrapevu @fikrapevu @fikrapevu

FIKRAPEVU MICHEZO

Jumatano Januari 01, 2025 Tovuti: www.fikrapevu.co.tz

# Huyu ndiye Clement Mzize usiyemjua

NA MWANDISHI WETU

**Hazungumzwi sana, lakini rekodi alizonazo ndani ya kikosi cha Yanga zinambeba, Clement Mzize aliyegeuka kuwa mshambuliaji hatari na muhimu wa kikosi hicho kilichopo chini ya kocha Sead Ramovic.**

Mshambuliaji huyo mzawa licha ya kuletewa mastaa wengi wa kigeni ndani ya timu hiyo, bado ameonekana kuuwasha na kubeba rekodi nzuri kuliko mastaa hao anaocheza nao nafasi moja Jangwani.

Akiwa na msimu wa tatu tangu alipopandishwa akitokea timu ya vijana, Mzize amezidi kuwa mtamu akimfunika hadi Kennedy Musonda anayelingana muda wa kuitumikia timu hiyo, akipita mikononi mwa makocha Nasreddine Nabi na Miguel Gamondi kabla ya kuja kwa Sead Ramovic.




Katika misimu mitatu ya Ligi rekodi zinaonyesha Mzize amemkimbiza Musonda ambaye amekuwa akiimbwa kwenye kikosi hicho, kwani amehusika katika mabao 25 (kabla ya mechi dhidi ya Fountain Gate FC), akifunga mabao 16 na asisti tisa, wakati Musonda akifunga jumla ya mabao 11 na asisti mbili ndani ya misimu hiyo mitatu kwa Ligi Kuu.

Katika msimu wa Mzize wa kwanza wa 2022/23 alikuwa sehemu ya kikosi kilichoipa timu hiyo taji la Ligi Kuu akifunga mabao matano na kutoa pasi moja iliyozaa bao, hivyo alihusika kwenye mabao sita kati ya mabao 43 yaliyofungwa na timu hiyo huku Fiston Mayele (Yanga) na Saidoo Ntibanzonkiza (Simba) wakiibuka wafungaji bora baada ya kupachika mabao 17 kila mmoja.

Kwa Musonda rekodi zinaonyesha msimu huo akiingia katika dirisha dogo, alifunga mabao manne bila ya asisti, ilihali katika msimu wao wa pili, Mzize alifunga mabao sita na kuasisti saba, akimuacha mbali Mzambia huyo aliyefunga mabao matano na asisti mbili.

Kwa msimu huu wakati Musonda ndio kwanza akianza kurejea tena kutoka kwenye majeraha

# Simba wampa 5 Fadlu

NA ELLY SARONGO

**PONGEZI KWAKE! Simba imempongeza kocha wa timu hiyo, Fadlu Davids na kusema, alichofanya katika mchezo wa juzi dhidi ya Kilimanjaro Wonderers alifanya kitu kizuri zaidi kwa kuwaamini wachezaji wake.**

Juzi, Simba ilikutana na Kilimanjaro Wonderers katika mchezo wa Kombe la Shirikisho la TFF, uliopigwa katika Uwanja wa KMC, Mwenge, Dar es Salam ambapo iliondoka na ushindi wa mabao 6-0 na kufanikiwa kuingia Raundi ya 32 Bora.

Akizungumza mara baada ya mchedzo huo, Meneja Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally alisema Fadlu amefanya kitu kizuri kwa kuwaamini wachezaji wake na kuwapa nafasi ya kucheza katika mchezo huo.

“Kwanza napenda kumpongeza Fadlu kwa kuwaamini wachezaji wake wote na kuwapa nafasi katika mchezo huu, pia huu ulikuwa mchezo muhimu kwa mashabiki ambao walikuja kuwapa shukrani wachezaji wao.



“Unajua timu imecheza mechi tatu na mashabiki hawakupata fursa ya kuwaona wachezaji wao, tulicheza Tunisia, Angola tukaja mechi ya Dar es Salaam na mechi zote tatu hizi hatukuwaona wachezaji wetu.

“Tunisia hatukuwepo, Angola hatukuwepo na Dar es Salaam tulikuwa tumekula ubaya ubwela, hivyo mashabiki walikuja ili kuwapongeza wachezaji wao kwa kazi kubwa waliyofanya.”